OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

SHULE YA SEKONDARI RELINI
S.L.P 42100, DAR ES SALAAM

SIMU0784 /0655–424258

relini42100@gmail.com

MTAAWAMTONI

KATAYAMTONI

Jina la mwanafunzi …….. No ya fomu ……..

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI RELINI WILAYA YA TEMEKE MKOA WA DAR ES SALAAM MWAKA……..

1.0 Ninafuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule yetu. HONGERA SANA. Shule ya Sekondari Relini , ipo kata ya Mtoni eneo la Mtongani, nyuma ya shule za msingi Bokorani na Mtoni, ipo hatua chache kutoka barabara kuuiendayo Mbagala.

Usafiri wa basi kutoka eneo lolote la Dar es Salaam unapatikana, panda basi la Mbagala au Mtongani na telemkia kituo cha Mtongani. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe ……, unatakiwa kuripoti shuleni tarehe …… **(fomu hii itunzwe kwa usafi na isikunjwe)**

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE YA SHULE

S/N	WAVULANA	WASICHANA
1.	**Suruali 2 za blue zisizobana au mlegezo.**	Sketi 2 za blue ndefu zinazovuka magoti mshono walinda boksi
2.	Mashati mawili (2) meupe yasiyo bana au mafupi au makubwa sana	Mashati mawili(2) meupe yasiyo bana au mafupi au makubwa sana
3	Soksi nyeusi jozi 2	Soksi nyeupe jozi 2
4	Mkanda mweusi wa ngozi usio na marembo au chuma kikubwa	Nusu kanzu na hijab nyeupe visivyo na urembo
5	Viatu vyeusi vya ngozi visivyo chongoka mbele, visivyo na marembo (viatu vinavyoruhusiwa ni four angle shoes)	Viatu vyeusi vya ngozi visivyo chongoka mbele, visivyo na marembo (viatu vinavyoruhusiwa ni four angle shoes)
6	Tie 2	Tie 2
7	Sare ya michezo ni jezi/ truck suit ya rangi ya "blue"	Sare ya michezo ni jezi/ truck suit ya rangi ya "blue"

2.2 VIFAA BINAFSI VYA MWANAFUNZI:

- Madaftari makubwa (Counter book 3 quire) 12.
- Seti ya vifaa vya Hisabati / Mkebe (Mathematical set) 1.
- Begi la kutunzia / kubebea daftari.
- Pocket dictionary English to English (Longman).

……..

JANATH R. MZEE

MKUU WA SHULE

KARIBU SANA SHULENI KWETU.

KIAMBATISHO A

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu, mafunzo ya Ufundi na sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

1. **MIPAKA YA SHULE.**

Ni wajibu wa kila mwanafunzi kujua eneo lote la shule na mipaka yake.Maeneo yafuatayo yanahesabika kuwa ni nje ya mipaka ya shule.

(a) Chumba cha walimu (staff room) na vyumba vya idara mbalimbali.
(b) Maabara ya sayansi
(c) Ofisi za Utawala
(d) Nyumba za walimu

Kwa kuwa shule hii ni ya kutwa,wanafunzi wanakaa sehemu mbalimbali za jiji la Dar es salaam,nje ya mipaka ya shule,kwa hiyo ipo haja ya kuwa na uhakika wa mahudhurio mazuri ya wanafunzi shuleni ili kudhibiti utoro na kuleta ufanisi shuleni.Hivyo basi mwanafunzi anapaswa kubaki Dar es salaam hata kwa siku ambazo si za masomo,isipokuwa wakati wa likizo kwa siku ambazo hana zamu au kazi ya shuleni.

2. **RUHUSA YA KUTOKA NJE YA MIPAKA YA SHULE AU NJE YA DAR ES SALAAM.**

(a)Ruhusa ya kutoka nje ya shule kwa muda tu au siku inatolewa na mwalimu wa darasa au mwalimu wa zamu kwa pasi(kibali maalumu)

(b)Ruhusa ya kutoka nje ya Dar es salaam itatolewa na makamu mkuu wa shule kwa pasi(kibali maalumu)

(c)Apatapo ruhusa ya nje ya shule,mwanafunzi anapaswa kuwahi kurudi.

(d)Ruhusa ya kwenda hospitali inapatikana kwa kupewa kibali na mwalimu wa darasa au mwalimu wa zamu.

3. NGUO RASMI ZA SHULE.

(a) Viatu vya ngozi nyeusi na visivyo na visigino virefu na vivaliwe na soksi kufuatana na maelekezo ya shule.

(b) Soksi fupi za rangi nyeupe wasichana na nyeusi kwa wavulana.

(c) T-shirt hairuhusiwi kuvaliwa ndani ya shati la shule. Vest (singlet)nyeupe inaruhusiwa kwa wavulana na brazia nyeupe kwa wasichana.

(d) Sweta ya rangi ya bluu.

II. UVAAJI WA SARE.
Sare ya shule itavaliwa katika mazingira yafuatayo:
(a)Wakati wa masomo

(b) Wakati wa likizo na siku za jumamosi wanafunzi wanapokuja shuleni

(c)Katika mikutano yote ya shule na mikutano ya hadhara.

III. UNADHIFU.
(a)Muda wote mwanafunzi awe nadhifu.
(b)Wavulana na wasichana wakate nywele ziwe fupi. (wasichana hawaruhusiwi kusuka)

4. MAHUDHURIO.

(a)Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo vya ndani na nje ya darasa kama ilivyoonesha kwenye ratiba.

(b)Wanafunzi wote wanatakiwa kuhudhuria na kushiriki katika shughuli zote za shule kama vile baraza la shule,ukaguzi wa usafi,kupandisha bendera ya Taifa na kazi za mikono.

(c)Ni lazima kutii kengele au wito wa shughuli yoyote ya shule kwa haraka na bila kuchelewa.

(d)Kuhudhuria zamu za kuja shule siku za mwisho wa wiki au likizo.

5. MALI NA VIFAA VYA SHULE.

Wanafunzi wote wanatakiwa kutunza kwa uwezo wao wote mali na vyombo vya shule vilivyo chini ya uangalizi wao.

(a)Hakuna chombo au kifaa cha aina yoyote kinachoruhusiwa kutoka mahalipake kwa matumizi au shughuli zisizo idhinishwa.

(b)Iwapo chombo kimehamishwa kwa shughuli maalumu nilazima kirudishwe mahali pake mara tu baada ya matumizi husika.

(c)Uharibifu au upotevu wa kifaa chochote cha shule kwa makusudi ama uzembe lazima ufidiwe na muhusika.

6. MATIBABU.

(a)Huduma ya kwanza itatolewa shuleni.

(b)Inapobidi kwenda nje ya shule kwa ajili ya matibabu ni lazima kuwe na ruhusa kutoka kwa mwalimu wa zamu.

(c)Shule haitawajibika na gharama zilizotumika /zitakazotumika kumtibu mwanafunzi katika zahanati/hospitali ya binafsi/serikali nje ya shule.

7. LUGHA YA MAWASILIANO.

Lugha rasmi kwa maandishi au kwa kuzungumza shuleni ni kingereza.Hivyo tumia kingereza wakati wote.

8. VITU VISIVYORUHUSIWA.

1.Pete
2.Kunyoa nyusi

3.Hereni
4.Kupaka hina
5.Rangi za kucha
6.Kucha ndefu
7.Kupaka piko (rangi nyeusi)kwenye nywele/upara
8.Kukali au kulilax ni marufuku
9.Hairuhusiwi kunyoa mitindo
10.Hairuhusiwi kunyoa vipara
11.Hairuhusiwi kuvaa mabuti na viatu vinavyofanana na jeshi
12.Hairuhusiwi kuvaa sandozi,mikanda isiyo endana na vazi rasmi la shule
13.Mashati makubwa sana na slim fiti hayaruhusiwi.
14.Simu ya mkononi hairuhusiwi
15.Huruhusiwi kuja na redio shuleni
16.Huruhusiwi kuja na "game"shuleni
17.Huruhusiwi kuja na CD wala Flash shuleni.

9. SHERIA YA JUMLA.

Kila wakati fikiria kwanza kabla ya kunena na tumia busara kutenda.

10.ADHABU.

(i) Adhabu zitaweza kutolewa na mwalimu yeyote kwa mwanafunzi anaye onesha utovu wa nidhamu.

(ii) Kiranja pia anaruhusiwa kutoa adhabu kulingana na kosa lililotendwa na mwanafunzi ilimradi asipige kiboko au kuzuia kuingia darasani wakati wa masomo.

(iii) Kosa linapokuwa kubwa litaandikwa katika jalada la mwanafunzi na kitabu cha kumbukumbu za adhabu.

11.MAKOSA HAYA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULENI BILA ONYO AU BILA KUJALI TABIA YAKO YA NYUMA.

1.Kuiba
2.Kufanya mapenzi
3.Ulevi wa aina yoyote
4.Uvutaji wa sigara,bangi na matumizi ya dawa zozote za kulevya

5.Kumpiga mwanafunzi,mfanyakazi au mtu wa familia ya mfanyakazi
6.Kudharau Bendera ya Taifa au wimbo wa Taifa au wimbo wa shule
7.Kuchochea mgomo wa aina yoyote au kufanya fujo ya kuhatarisha amani au usalama penye kundi la watu
8.Kukataa adhabu ya viboko
9.Kutofanya mitihani ya shule au Taifa
10.Kunyanyasa mwanafunzi kwa sababu ya ugeni wake au jinsia yake au umbile lake au dini yake
11.Kukataa kutii amri au adhabu iliyotolewa na Mkuu wa shule
12. Mwanafunzi haruhusiwi kulala ndani ya chumba cha mtihani au kutoka chumba cha mtihani kabla ya muda kuisha wa mtihani uliopangwa.

MWENENDO MWEMA NA NIDHAMU:

1. Msalimu mwalimu kwa heshima wakati wowote unapoonana naye hasa kwa mara ya kwanza kwa siku hiyo ukiwa umesimama..

2.Mwanafunzi asimame wakati mwalimu ama mtu yeyote anaye mzidiumri anapita au kuingia darasani.

3.Usizungumze na mwalimu au mtu yeyote anaye kuzidi umri wakati mikono iko mifukoni ama umevaa kofia kichwani au ikiwa umevaa miwani ya jua au kutafuna kitu mdomoni.

4.Usibishane na mwalimu au kiongozi yoyote bila sababu maalumu.Uamuzi wa mwalimu ni wa mwisho.

5.Usifanye kelele za fujo au ghasia katika sehemu zinazohitaji ukimya kama vile darasani,maktaba na kwenye gwaride.

6.Usiwe mchafu kimwili au kimavazi,uwe na nywele fupi bila kunyoa kipara,ndevu au masharubu zinyolewe kwa wembe.Uwe nadhifu.

7.Usitumie sigara,bangi na usitumie madawa ya kulevya na usinywe pombe.

8.Timiza wajibu au kazi uliyopangiwa.

9.Usitumie lugha ya matusi,na kusuka mitindo isiyokubalika.

10.Onesha heshima kwa walimu,raia na wengine wote.

11.Usiwe ndani au karibu ya vilabu,baa ya pombe hata kama hunywi pombe.

12.Usiandike mahali pasipo husika kama vile ukutani,vitabuni,kwenye samani za shule n.k.

13.Usimpige au kumshambulia mwanafunzi mwenzako ama hata mtu mwingine yeyote.

14.Usikatae uteuzi wa kushiriki shughuli mbalimbali kama vile michezo,maandamano,uwakilishi n.k

15.Usichelewe shule kutoka likizo na usizidishe siku za ruhusa ya kuwa nje ya shule,mwanafunzi akikosa kuhudhuria shule zaidi ya siku tatu mfululizo atalazimika kufika pamoja na mzazi au mlezi aliye andikishwa.

16.Usigune wala kuzomea wakati mwalimu au kiongozi yeyote anapotoa matangazo.

17.Usibandike tangazo lolote bila ruhusa ya mwalimu anaye husika na mada ya tangazo hilo.

18.Hotuba zote lazima zionwe na mkuu wa shule ,kabla ya kutolewa katika hadhara yoyote shuleni.

19.Usifanya mkutano bila ya ruhusa ya mwalimu anaye husika kukilea kikundi kinacho husika.

20.Usihubiri dini,siasa au jambo lolote.Sala zote zifanyike mahali panapo husika kama vile kanisani au msikitini.

KIAMB\ATISHO D:

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA AHADI

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI RELINI,
S.L.P 42100
DAR ES SALAAM

KWA MWANAFUNZI

MIMI……..(Jina kamili)
Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha…… mwaka……katika shule……sekondari.
NINAAHIDI KWAMBA:

1. Nitatii sheria za shule kama nilivyosoma
2. Nitaweka bidii katika masomo, kazi na shughuli zote za shule.
3. Nitashiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali, kuzalisha mali iliyo bora bila kuitia hasara shule kwa uharibifu au kupoteza malighafi (raw materials ya uzalishaji mali)
4. Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu mkakamavu na mwenye mwenendo safi wakati wowote hata nikiwa nje ya shule kwa madhumuni ya kuipa na kutunza sifa ya shule ya……sekondari.

MUNGU NISAIDIE.
Saini ya mwanafunzi……

KWA MZAZI/ MLEZI.

Mimi……
Ninaahidi kwamba:

1. Nitampatia mwanangu mahitajiya shule kama yalivyotajwa katika maelezo ya kujiunga shule.
2. Nitakuwa tayari kutoa msaada wowote utakaohitajika (maoni, adhabu) katika kumlea mwanangu.
3. Nitamhimiza mwanangu kufanya mazoezi yake ya masomo nyumbani (home work) na kufuatilia maendeleo yake na tabia yake shuleni.
4. Mwanangu akiwa nyumbani nitamtunza na kumwangalia vizuri mwenendo wake

Saini ya mzazi/ mlezi…….

KIAMBATISHO B:

OFISI YA RAIS

SHULE YA SEKONDARI……

FOMU YA KUANDIKISHWA SHULE.

PICHA YA MWANAFUNZI

A:**IJAZWE NA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili la mwanafunzi……..
2. Tarehe ya kuzaliwa…….
3. Taifa……
4. Uraia……
5. Dini……
6. Shule alizosoma kabla ya kuja shule ya sekondari……
   ……

Shule ya msingi	Tarehe na mwaka aliomaliza	Tarehe na mwaka aliotoka
I		
II		
III		
IV		

Saini ya Mwanafunzi……

B: **MAELEZO BINAFSI YA MZAZI/MLEZI**

1. Jina kamili la Mzazi/ Mlezi……
2. Utaifa……..
3. Uraia……
4. Anuani ya Mzazi/Mlezi…….
5. Sehemu anayoishi…….
6. Mtaa…….
7. Namba ya nyumba……
8. Simu: Nyumbani……

   Ofisini……

PICHA YA

MZAZI/MLEZI

C: **MAELEZO YA KIKAZI**

I. Jaza jina la mwajiri……..

II. Anuani……

III. Kazi ya Mzazi/ Mlezi……..

IV. Saini ya Mzazi/ Mlezi……

KIAMBATISHO C

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

STATION…….

DATE……

PART A:

TO

Medical officer

……..

……

Miss/ Mr…….

Please examine the above named as to his / her fitness for admission as a student in the following common diseases/ problems:-

Put a tick **(v)** for positive and a cross **(x)** for negative in a box provided

Pregnancy	
Asthma	
Diabetes	
Worms(stool)	
Epilepsy	
TB (Tuberculosis)	
Sickle Cell	
Heart Disease	
Yellow Fever	
U.T.I	
Malaria	

PART B: **MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Medical Officer)

I have examined the above named and consider that she / he is physically FIT/ UNFIT for admission above.

Date…… Signature……

Station……\. Designation……..